# Wasri Lanka wanausaka ulimwengu ambamo wataweza kupata kicheko kwa pamoja:Jarida la Thelasini na Moja (2022).



Anoli Perera (Sri Lanka), Dream 1, 2017.

Marafiki wapendwa,

Salamu kutoka katika dawati la Tricontinental: Institute for Social Research.


Mnamo tarehe 9 Julai 2022, taswira za kustaajabisha zilizagaa katika mitandao ya kijamii kutoka Colombo,mji mkuu wa Sri Lanka. Maelfu ya watu waliingia katika kasri la Rais na kumtimua Rais wa zamani Gotabaya Rajapaksa, hali iliyomlazimisha kukimbilia nchini Singapore. Mwezi Mei, kaka wa Gotabaya aitwaye Mahinda ambaye naye ni Rais wa zamani, alijiudhuru kutoka katika wadhifa wake wa Uwaziri Mkuu na kukimbia yeye na familia yake kwenda katika kambi ya jeshi la wanamaji ya Trincomalee. Hasira mbichi ya umma dhidi ya familia ya Rajapaksa haikuweza tena kuzuiwa,na mizizi ya kina Rajapaksa ambayo iilinasa dola kwa miaka mingi, iliong’olewa.

Sasa, takribani mwezi mmoja baadaye,masalia ya hisia kutoka katika maandamano yamebaki lakini hayajafaulu kuleta madhara muhimu.

Rais mlezi mpya wa Sri Lanka,Rais Wickremesinghe, ameongeza muda wa hali ya hatari na kuviamuru vikosi vya ulinzi kulivunja eneo la Galle Face Green Park ambalo ni eneo la kufanyia maandamano (likiitwa kwa umashuhuri Gotagogama).

Kupanda kimadaraka kwa Wickremesinghe kwenye urais kunadhihirisha kwa kiasi kikubwa juu ya udhaifu wa vuguvugu la maandamano katika nchi hii yenye watu 22 milioni na uimara wa tabaka tawala la Sri Lanka.Katika bunge chama cha Wickremesinghe cha United National Party kina kiti kimoja tu – chake yeye mwenyewe – ambacho alikipoteza mwaka 2020.Ila amekuwa Waziri Mkuu wa serikali sita akiingia na kutoka tangu mwaka 1993 mpaka leo,hajawahi kamwe kumaliza muhula akiwa ofisini,lakini ameendela kuzikamata hatamu kwa niaba ya tabaka tawala.

Zamu hii bwana Wickremesinghe amengia madarakani kupitia chma cha kina Rajapaksa cha Sri Lanka Podujana Peramuna (Sri Lanka People’s Front),ambacho kilitumia wabunge wake 114( katika bunge lenye watu 225)  kuunga mkono usimikwaji wake katika ofisi kuu zaidi katika nchi ile.Kwa maneno mengine familia ya Rajapaksa imejiuzulu kwa urasmi,ila nguvu yao -kwa niaba ya wamiliki wa nchi -itasalia.



Sujeewa Kumari (Sri Lanka), Landscape, 2018.

Watu waliokusanyika Galle Face Green Park na maeneo mengine nchini Sri Lanka waliandamana sababu ya hali ya uchumi visiwani mle ambayo ilikuwa haistahimiliki tena.

Hali ilikuwa mbaya kiasi, mwezi Machi 2022 , serikali ililazimika kufuta zoezi la mitihani katika shule sababu ya ukosefu wa karatasi. Bei za bidhaa zilipanda, huku bei ya mchele , chakula kitumikacho kwa wingi, ikipaa kutoka rupia 80 za Sri Lanka (LKR) mpaka 500 LKR, matokeo ya ugumu katika uzalishaji sababu ya upungufu wa umeme, mafuta, na mbolea.

Maeneo mengi ya nchi (isipokuwa kanda maalumu za kibiashara)yalikumbwa na 'mgao wa umeme' kwa angalau nusu siku,kila siku.

Tangu Sri Lanka ilipopata uhuru wake kutoka kwa waingereza mwaka 1948, tabaka lake tawala limekumbana na janga juu ya janga ambayo yanatokana na utegemezi wa kiuchumi kwa usafirishaji nje wa mazao ya kilimo,zaidi yakiwa ni mpira,chai, na, Kwa kiasi kidogo,mavazi. Majanga haya hususani ya mwaka 1953 na 1971 – yalipelekea kuangushwa kwa serikali zilizokuwa madarakani. Katika mwaka 1977, tabaka la wachache waliamua kuufanya uchumi kuwa wa kiliberali kwa kuondoa udhibiti wa bei na ruzuku za chakula na kuruhusu benki za nje na

uwekezaji wa nje kufanya kazi pasi udhibiti makini. Waliunda walichokiita Kamisheni ya Kiuchumi ya Colombo Kuu mwaka 1978 ili wachukue vilivyo udhibiti wa uchumi wa nchi nje ya utaratibu wa udhibiti wa kidemokrasia.

Madhara ya mipango hii ya kiliberali mamboleo yalikuwa ni kunawiri kwa deni la taifa(ballooning of the national debt),ambalo lilikuwa likizunguka tu huku na kule lakini lisiweze kuingia katika hali/eneo salama. Kasi ndogo ya ukuaji sambamba na mtindo wa kutoa dhamana za madeni ya nje kulipia mikopo ya nyuma zimefifisha namna zote za kutegemeza uchumi. Mwaka 2020, S&P Global Ratings iliipunguzia alama Sri Lanka kutoka alama B-/B mpaka CCC+/C, alama ndogo zaidi juu ya alama D ambayo 'ni kama alama ya 'hadhi ya lazima' katika kuhimili mikopo ya nje kwa muda mrefu.



Thamotharampillai Sanathanan (Sri Lanka), Jaffna, 1990–95.

Tabaka tawala la Sri Lanka limekuwa likishindwa,ama labda kutokuwa na nia, kupunguza utegemezi kwa wanunuzi wa nje wa bidhaa zake za thamani ya chini pamoja na wakopeshaji wanaoliruzuku deni lake.

Kwa nyongeza,kwa miongo kadhaa iliyopita -hususani tangu mwaka mbaya wa maandano ya Colombo 1983 – tabaka la wachache nchini Sri Lanka walizidisha matumizi makubwa katika shughuli za jeshi,huku wakivitumia vikosi hivi kutekeleza mauaji ya kutisha ya jamii ya wachache ya Tamil. Bajeti ya nchi kwa mwaka huu 2022 imetenga  12.3% ya mapato kwa matumizi ya ya serikali kwa jeshi. Ukitizama namba ya idadi ya wanajeshi kwa kulinganisha na idadi ya jumla ya raia,Sri Lanka (1.46%) inaifuatia Israel (2%) inayoongoza kidunia, na kuna mwanajeshi mmoja katika kila raia sita kwenye majimbo ya Kaskazini na Mashariki ya visiwa vile,maeneo ambayo wanapatikana watu wa jamii ya Tamil. Aina hii ya matumizi,makubwa yanaipekea jamii ya Sri Lanka kufanywa jamii ya kijeshi.

Wamiliki wa deni la taifa ni wengi,lakini wajibu mkubwa ni lazima uangukie kwa tabaka tawala la Sri Lanka na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF).

Tangu mwaka 1965,Sri Lanka imetafuta usaidizi toka IMF mara kumi na sita.Katika kina cha mtatizo ya sasa,mwezi Machi 2022,Bodi ya wakurugenzi ya IMF ilipendekeza  kwamba Sri Lanka ipandishe kodi ya mapato,iuze mashirika ya umma,na kuondoa ruzuku katika sekta ya nishati na bidhaa zake. Miezi mitatu baadaye,baada ya degedege ya uchumi iliyojitokeza kuunda mgogoro mkubwa wa kisiasa, maofisa wa IMF waliozuru Colombo na walijumuisha ziara yao kwa kutoa wito kufanyike mageuzi zaidi ,hususani kwa kutumia mbegu ileile ya 'ubinafsishaji'. Balozi wa Marekani nchini humo Julie Chang alikutana na Rais Wickremesinghe na Waziri Mkuu Dinesh Gunawardena na kusaidia 'mazungumzo yao na IMF'.

Hakukuwepo na kujali kwa aina yeyote juu ya suala la hali ya hatari wala hali mbaya ya kisiasa.



Chandraguptha Thenuwara (Sri Lanka), Camouflage, 2004.

Vikao hivi vinaonesha kiwango ambacho Sri Lanka imeburuzwa bila hiyari na Marekani katika “vita mseto” vyake dhidi ya China,ambayo uwekezaji wake umekuwa ukikuzwa (kutiwa chumvi) ila kuhamisha lawama kuhusu janga la deni la taifa kutoka kwa viongozi wa Sri Lanka na IMF. Takwimu rasmi zinaonesha kuwa ni 10% tu ya deni la nje nchini Sri Lanka linadaiwa na taasisi za kutoka China, ilhali 47% ya deni la nje likishikiliwa na benki na makampuni ya uwekezaji ya mataifa ya magharibi kama vile BlackRock, JP Morgan Chase, na Prudential (Marekani), sambamba na Ashmore Group na HSBC (Uingereza) na UBS (Uswisi).

Licha ya haya, IMF na USAID wanatumia lugha inayoshabiiana,wakiendela kusisitiza kuwa ni muhimu kujadiliwa upya kwa deni lililopo baina ya Sri Lanka na China.Hata hivyo, tuhuma chafu kuwa China inatumia “diplomasia ya mtego wa madeni” zinakosa msingi Kama ilivyooneshwa katika uchunguzi uliochapishwa na *The Atlantic*.

Wickremasinghe amekaa katika nyumba ya Rais akiwa na ajenda iliyoshindwa.Ni muumini kindakindaki wa mradi wa Washington,akitamani kusaini mkataba wa mashirikiano ya kijeshi na Marekani ili aimarishe jeshi,na alikuwa tayari kwa Sri Lanka kujiunga na mpango wa malengo ya millenia (MCC) uliambatana na msaada wa fedha kiasi cha dola za kimarekani milioni 480.Hata hivyo,moja kati ya sababu zilizopelekea chama cha Wickremesinghe kushindwa vibaya katika uchaguzi ni ukinzani mkubwa wa wapiga kura dhidi ya sera hizo zote uliojitokeza.Sera hizo ziliundwa kwa mtindo kuisogeza Sri Lanka katika ushirika dhidi ya China ambayo ungenyausha uwekezaji wa lazima wa China.Wasri Lanka wengi wanatambua kuwa hawastahili kuburuzwa katika mgogoro unaokua baina ya Marekani na China ama katika mgogoro wa kale ambao bado mbichi-wa kijamii mbalimbali katika nchi yao ambao -unapaswa kutibiwa.



Jagath Weerasinghe (Sri Lanka), Untitled I, 2016.

Muongo uliopita, rafiki yangu Malathi De Alwis (1963–2021), pofesa wa Chuo Kikuu Cha Colombo, alikusanya mashairi yaliyoandikwa na wanawake wa Kisri Lanka.Nilipokuwa nikisoma,

nilistàajabia kukutana na maneno ya Seetha Ranjani ya mwaka 1987. Kwa kumbukumbu ya Malathi na kuunga mkono tumaini la Ranjani,hii hapa ni dondoo ya shairi liitwa “Ndoto ya Amani”:

Huwenda mashamba yetu yaliounguzwa moto bado yana thamani
Kama mapya ama zaidi
Huwenda amani pia inaweza kuagizwa -kama bidhaa toka nje

Ila kuna chochote kinachoweza kufuta maumivu yaliyoletwa na vita?
Tizama katikati mabaki ya uharibifui:tofali baada ya tofali
Mikono ya watu ilifanya kazi kujenga maskani ile
Pepesa macho yako yenye udadisi katika kifusi
Kesho ya wanetu imeteketzwa pale

Yupo awezaye kupima thamani ya nguvu -kazi iliyopotea?
Yupo awezaye kupuliza pumzi ya uhai kwa maisha yaliyoharibiwa?
Viungo vya miili vilivyovunjwa vinaweza kuundwa upya?
Ufahamu wa watoto waliozaliwa na ambao hawajazaliwa waweza kuundwa upya?

Tulikufa –
na tunakufa,
Tulizaliwa upya
Tulia
na tunalia,
Tulijifunza kutabasamu tena
Na sasa –
Hatutafuti tena maswaiba wa kulia nasi tuliapo.
Badala yake,tunatafuta ulimwengu ambao tutaweza kupata kicheko kwa pamoja.

Kwa huba,

Vijay